**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621** **KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Jumatatu, 07 Mei 2007 mchana**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Eleza hatua nne ambazo mwalimu anapaswa kufuata wakati wa kufundisha msamiati mpya.
2. Taja sifa nne zinazotofautisha tamthilia na riwaya katika fasihi ya Kiswahili.
3. Toa hoja nne kuthibitisha umuhimu wa mashairi ya Kiswahili katika kukuza maadili ya jamii.
4. Eleza tofauti kati ya hotuba rasmi na hotuba isiyo rasmi.
5. Bainisha mambo manne yanayomsaidia mwanafunzi kuandika insha yenye mvuto.
6. Eleza nafasi ya hadithi za jadi katika malezi ya watoto wa Kitanzania.
7. Eleza kwa ufupi vigezo vinne vya kuchagua vitabu vya kiada shuleni.
8. Toa faida nne za kujifunza Kiswahili kupitia michezo ya lugha.
9. Eleza umuhimu wa mitihani ya majaribio (mock) kwa wanafunzi.
10. Taja mambo manne yanayojitokeza katika maandiko ya lugha ya Kiswahili ya kimaandishi.

**SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Jadili nafasi ya methali katika kujenga mshikamano wa kijamii.
12. Kwa hoja tano, eleza faida za mwanafunzi kushirikiana na wenzake katika kujifunza lugha.
13. Eleza hatua nne zinazohusiana na maandalizi ya mwalimu kabla ya kuingia darasani.
14. Kwa hoja tano, thibitisha umuhimu wa fasihi simulizi katika kukuza utamaduni wa taifa.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

15. Eleza sifa tano zinazohitajika katika maandiko bora ya kitaaluma.

16. Toa faida tano za mwalimu kutumia mbinu mchanganyiko za ufundishaji darasani.

17. Jadili mbinu tano zinazowasaidia wanafunzi kujenga uwezo wa kujieleza kwa ufasaha.

18. Eleza matatizo matano ambayo mwalimu anaweza kukutana nayo anapotumia vitini kama zana za kufundishia.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org